MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na. 18 Toleo maalumu: Utabiri wa mvua za msimu wa Vuli (Oktoba hadi Disemba), 2017** **04 Septemba, 2017**

**MUHTASARI**

- Utabiri wa mvua za Oktoba hadi Disemba, (Vuli) ni mahususi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Utabiri wa mvua katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua utatolewa mwezi Oktoba.
- Mvua za vuli zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Kagera, Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, mashariki mwa mkoa wa Arusha, Manyara, kaskazini mashariki mwa mkoa wa Pwani pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.
- Mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Arusha, Manyara, Pwani, Tanga, kaskazini mwa mikoa ya Kigoma (wilaya ya Kibondo) na Morogoro.
- Mvua za vuli zinatarajiwa kuanza mwezi Septemba katika maeneo ya ukanda wa ziwa Viktoria, Oktoba kwa maeneo ya ukanda wa pwani, na Novemba kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki.
- Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba mapema na kupanda mazao yanayokomaa katika muda mfupi pamoja na kupata ushauri wa wataalamu wa kilimo katika maeneo yao.
- Wafugaji wanashauriwa kuwa na mifugo inayolingana na uwezo wa malisho yaliyopo pamoja na kuzingatia ushauri wa maafisa kilimo na mifugo katika maeneo yao.

## MWELEKEO WA MIFUMO YA HALI YA HEWA: OKTOBA - DISEMBA, 2017

Hali ya joto la juu ya wastani iliyopo magharibi mwa Bahari ya Hindi inatarajiwa kuendelea katika kipindi cha Oktoba-Disemba. Kwa upande mwingine hali ya joto la wastani inatarajiwa katikati mwa eneo la Kiikweta la Bahari ya Pasifiki. Katika kipindi cha msimu wa Vuli, hali ya joto la chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola).

Vipindi vya migandamizo midogo ya hewa vinatarajiwa kujitokeza katika eneo la pwani ya Somalia hivyo kuchelewesha kuhama kwa ukanda wa mvua kuelekea kusini mwa Ikweta. Hali hiyo, inatarajiwa kusababisha kuchelewa kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli. Vimbunga vinatarajiwa kujitokeza katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hivyo kupeleka upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Kongo na kuingia nchini. Hali hii ya upepo kutoka katika misitu ya Kongo inatarajiwa kusababisha vipindi vya ongezeko la mvua katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

## MWELEKEO WA MVUA: OKTOBA –DISEMBA, 2017

Msimu wa mvua wa Vuli ni mahususi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Ukanda wa ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki, visiwa vya Unguja na Pemba, pwani ya kaskazini na maeneo ya kaskazini mwa mikoa ya Kigoma (Kibondo) na Morogoro) kama inavyoonekana kwenye Kielelezo.


Mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza mwezi Septemba katika maeneo mengi ya Ziwa Viktoria na mwezi Oktoba katika ukanda wa pwani, na baadaye mwezi Novemba katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika miezi ya Novemba na Disemba, na vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza zaidi mwezi Oktoba.

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga):** Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza mapema, kati ya wiki ya pili na tatu ya mwezi Septemba kwa maeneo ya mkoa wa Kagera na kusambaa mikoa ya Geita, Mwanza, Mara, Simiyu na Shinyanga ifikapo wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Oktoba. Mvua hizo zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Shinyanga na Simiyu na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika mkoa wa Kagera. Mvua za msimu wa Vuli zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba katika maeneo mengi ya Ziwa Viktoria, isipokuwa baadhi ya maeneo ya mkoa wa Mwanza ambapo mvua zinatarajiwa kuisha mapema katika wiki ya tatu ya mwezi Disemba.

**Ukanda wa pwani ya kaskazini: (Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro):** Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi

Oktoba. Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi isipokuwa maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro na maeneo mengi ya mkoa wa Pwani ambayo yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Mvua katika maeneo tajwa zinatarajia kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba.

**Nyanda za juu Kaskazini Mashariki: (Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Manyara na Arusha. Hata hivyo, mkoa wa Kilimanjaro unatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani. Mvua hizi zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba.




Kielelezo: Mwelekeo wa mvua za msimu wa *Vuli,* 2017

## ATHARI NA USHAURI

**Kilimo, mifugo, wanyamapori na uvuvi**

Hali ya unyevu wa udongo kwa ajili ya mazao na malisho ya mifugo na wanyamapori inatarajiwa kuwa ya kuridhisha hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba yao mapema na kupanda mazao yanayokomaa katika muda mfupi kwa kufuata ushauri wa wataalam wa kilimo. Wafugaji wanashauriwa kuvuna mifugo yao ikiwa katika hali nzuri na pia kuvuna maji na kuhifadhi malisho ili kukidhi mahitaji katika kipindi cha upungufu.

Upungufu wa unyevunyevu unatarajiwa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kupanda mazao kukomaa kwa muda mfupi na yanayostahimili mvua chache na kufuata ushauri wa wataalam. Uzalishaji wa samaki katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani unatarajiwa kuongezeka, wakati katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani uzalishaji unatarajiwa kupungua. Wavuvi na wafugaji wa samaki wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa uvuvi.

**Menejimenti za Maafa**

Mamlaka zinazoshughulika na maafa zinashauriwa kuweka mipango na maandalizi mazuri juu ya hatua stahiki zitakazotakiwa kuchukuliwa kutokana na madhara yanayoweza kusababishwa na mvua zinazotarajiwa.

***Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mwelekeo wa mvua nchini. Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Wadau wa sekta ya kilimo na mifugo, wakiwemo wakulima wanashauriwa pia kufuatilia tabiri za saa 24, siku 10 pamoja na za mwezi kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Mamlaka ya Hali ya Hewa inawashauri pia watumiaji wa taarifa za hali ya hewa waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo, uvuvi na mifugo katika maeneo yao.***

*Linatayarishwa na:*
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3, 4 na 10 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro .
*S.L.P 3056 Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8 ; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 Baruapepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet1_tz@meteo.go.tz*
Dar es Salaam JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA